

Unapaswa Kufanya Nini?

Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa. Kumbuka kwamba hakuna majibu yasiyo sahihi. Tafadhali fikiria kwa makini kuhusu maswali haya na ushiriki maoni yako binafsi.

Tukio la 1

Sofia na rafiki yake wa karibu Joaquín wametoka kuwa na ugomvi mkubwa. Baadaye, Sofia ameshiriki chapisho la kudunisha kumhusu Joaquín kwenye mtandao wa kijamii. Baadaye usiku, Joaquín anamtumia ujumbe na wanasameheana lakini chapisho lake bado lipo mtandaoni.

- Nini ingeweza kutokea?
- Sofia anapaswa kufanya nini? Joaquín anapaswa kufanya nini?
- Je, unaweza kufikiri kuhusu mfano halisi wa hali kama hii?

Tukio la 2

Daudi alipiga picha za baadhi ya marafiki zake wakifanya mambo ya kijinga kisha akazichapisha kwenye mitandao ya kijamii, akitumia alama za reli ambazo zingesikika kuwa za kifidhuli au za kudhalilisha, lakini hakika zilikuwa mizaha pamoja na marafiki zake. Keshoye, Catalina na rafiki mwingine walimwendea Daudi shuleni na kumwambia kwamba anafiriki kwamba alama za reli hizo ziliwaumiza sana na kwa namna fulani zilikuwa za kingono (yaani, maonevu au ubaguzi kwa misingi ya kijinsia; hasa ubaguzi dhidi ya wanawake).

- Nini ingeweza kutokea?
- David anapaswa kufanya nini? Catalina angeweza kufanya nini kingine?
- Je, ingekuwaje iwapo Catalina angemkabili Daudi mtandaoni badala ya kumkabili moja kwa moja?
- Je, unaweza kufikiri kuhusu mfano halisi wa hali kama hii?
- Je, iweje Catalina angeanza kumrejelea kama mwonevu? Je, unadhani kuonekana kwa Daudi kuwa mwonevu kungeathiri vipi sifa yake siku za usoni?

Tukio la 3

Aditi alikuwa kwenye mitandao ya kijamii alipogundua kuwa Mary, msichana wa shule, alipiga picha yake (Aditi) kisha akaandika, “Haha #whatnottowear” (akikejeli mavazi yake). Bila shaka, Aditi aliudhika sana.

- Je, nini kingeweza kutokea?
- Je, Mary anafaa kufanya nini? Aditi anapaswa kufanya nini?

Unapaswa Kufanya Nini? Nakala ya Mwalimu

Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa. Kumbuka kwamba hakuna majibu yasiyo sahihi. Tafadhali fikiria kwa makini kuhusu maswali haya na ushiriki maoni yako binafsi.

Tukio la 1

Sofia na rafiki yake wa karibu Joaquín walitoka kuwa na ugomvi mkubwa. Baadaye, Sofia ameshiriki chapisho la kudunisha kumhusu Joaquín kwenye mtandao wa kijamii. Baadaye usiku, Joaquín anamtumia ujumbe na wanasameheana lakini chapisho lake bado lipo mtandaoni.

- Nini ingeweza kutokea?
- Sofia anapaswa kufanya nini? Joaquín anapaswa kufanya nini?

Huenda mtu angeona chapisho hilo na kumripoti Sofia kuwa mwonevu au kufasiri vibaya uhusiano wake na Joaquín na hisia zao kuelekea mwingine. Huenda Joaquín bado angeona chapisho hilo kuwa la kifidhuli. Pengine ni jambo jema kwa Sofia kuondoa chapisho lake.

- Je, unaweza kufikiri kuhusu mfano halisi wa hali kama hii?

Washiriki wanaweza kutafakari kuhusu mifano ambayo wamepitia au kusikia kuhusu siku zilizopita. Kumbuka kwamba kushiriki mifano hii halisi huenda kukawakera washiriki. Waambie washiriki mifano ya marafiki au watu wanaowafahamu (dhidi yao).

Tukio la 2

Daudi alipiga picha za baadhi ya marafiki zake wakifanya mambo ya kijinga, kisha akazichapisha kwenye mitandao ya kijamii, akitumia alama za reli ambazo zingelikika kuwa za kifidhuli au za kudhalilisha, lakini hakika ulikuwa ni utani tu pamoja na marafiki zake. Keshoye, Catalina na rafiki mwingine walimwendea Daudi shuleni na kumwambia kwamba anafiriki kwamba alama za reli hizo ziliwaumiza sana na kwa namna fulani zilikuwa za kingono (yaani, maonevu au ubaguzi kwa misingi ya kijinsia; hasa ubaguzi dhidi ya wanawake).

- Nini ingeweza kutokea?
- David anapaswa kufanya nini? Catalina angeweza kufanya nini kingine?

Daudi anapaswa kuomba msamaha au ajieleze. Washiriki wanapaswa kuzingatia jinsi hatua zao zinaweza kuchukuliwa tofauti na jinsi walivyolenga, lakini hilo halina maana kwamba mitazamo mingine si sahihi.

- Je, ingekuwaje iwapo Catalina angemkabili Daudi mtandaoni badala ya kumkabili moja kwa moja?

Ikiwa Catalina angemkabili Daudi kwenye chapisho la umma, watu wengine wangeweza kuchangia suala hilo na kueleza mzaha fiche au kwa nini kauli hiyo ilikuwa ya kuudhi. Inaweza kusuluhishwa au inaweza kuwa mzozo mkubwa miongoni mwa watu wengine. Ikiwa Catalina angewasiliana na Daudi kupitia ujumbe mtandaoni, basi Daudi angeweza kujadili jambo hilo naye baadaye na kubadilisha chapisho lake ikiwa angeshawishika kwamba halikufaa.

- Je, unaweza kufikiri kuhusu mfano halisi wa hali kama hii?

Washiriki wanapaswa kutafakari kuhusu jinsi walivyotatua matukio ya kutowasiliana ipasavyo hapo awali. Kumbuka kwamba kushiriki mifano hii halisi huenda kukawakera washiriki. Waambie washiriki mifano ya marafiki au watu wanaowafahamu (dhidi yao).

- Je, iweje Catalina angeanza kumrejelea kama mwonevu? Je, unadhani kuonekana kwa Daudi kuwa mwonevu kungeathiri vipi sifa yake siku za usoni?

Washiriki wanapaswa kutafakari kuhusu maana ya kuwa mwonevu na wazingatie jinsi maudhui mtandaoni yanaweza kuathiri jinsi marafiki wanarika wanavyowachukulia.

Tukio la 3

Aditi alikuwa kwenye mitandao ya kijamii alipogundua kuwa Mary, msichana wa shule, alipiga picha yake (Aditi) kisha akaandika, “Haha #whatnottowear” (akikejeli mavazi yake). Bila shaka, Aditi aliudhika sana.

- Je, nini kingeweza kutokea?
- Je, Mary anafaa kufanya nini? Aditi anapaswa kufanya nini?

Aditi anapaswa kumkabili Mary kuhusu vitendo vyake ili amjulishe kwamba hatua hizo zinaumiza. Pia Aditi anaweza kuripoti vitendo vya Mary kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii na mtu mzima (k.m., mzazi / mtunzaji, mwalimu au msimamizi wa shule).